

# **TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**Katika ujumbe wa kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ahimiza vijana wahakikishe sauti zao zinasikika, na kuona kwamba wakuu wa nchi duniani wanatekeleza ahadi za kupambana na umaskini**

Ufuatao ni ujumbe wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa Kofi Annan kuhusu siku ya Vijana Duniani inayoadhimishwa tarehe 12 Agosti:

Hivi sasa, kuna takriban watu bilioni 3 duniani walio chini ya umri wa miaka 25. Zaidi ya nusu bilioni kati yao wanaishi maisha ya kiwango cha chini ya dola mbili kwa siku. Zaidi ya watoto milioni 100 waliofikia umri wa kwenda shule hawako shuleni. Karibu watoto 30,000 hufa kila siku kutokana na umaskini. Na vijana 7,000 huwa wameambukizwa UKIMWI.

Hali hiyo inaweza kubadilika, endapo tutashirikiana kufanya kazi kwa pamoja ili kufanikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia.

Malengo hayo yalipitishwa miaka mitano iliyopita na Serikali zote duniani kama mwongozo wa kujenga dunia iliyo bora zaidi katika karne ya 21. Yanawakilisha ushirikiano.

Nchi maskini zimeahidi kujenga utawala bora zaidi, na kuwekeza rasimali katika watu wao kwa njia ya huduma bora za afya na elimu.

Nchi tajiri zimeahidi kuzisaidia nchi maskini kwa njia ya misaada, unafuu wa madeni, na masharti mazuri ya biashara.

Mwezi ujao, Viongozi wa Mataifa na Wakuu wa Serikali watakutana huko Umoja wa Mataifa kwa ajili ya Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa 2005 – unaotarajiwa kuwa mkusanyiko mkubwa kupindukia wa viongozi ambao haujawahi kutokea. Naamini tutakuwa na fursa ya kipekee ya kizazi hiki ya kushughulikia baadhi ya changamoto kubwa katika uhai wetu.

Inabidi viongozi wakumbushwe ahadi yao ya kuhakikisha Malengo ya Maendeleo ya Milenia yanatekelezwa. Hapo ndipo vijana kama nyie mnapaswa kuhusika. Sauti zenu zinaweza kuwakumbusha viongozi hao kuhusu ahadi zao – katika mkutano wa Wakuu wa Nchi wa 2005 na hata siku zijazo.

Natambua kuwa hamuwezi kukubali kuishi katika dunia ambamo wengine wanakufa kwa njaa, wanabaki na ujinga wa kutojua kusoma na wanapoteza heshima yao.

Hivyo basi, hakikisheni sauti zenu zinasikika. Hakikisheni kuwa kizazi chenu ndicho cha kuutokomeza kabisa umaskini.